Tangazo la Serikali. ………………… la tarehe …………………

SHERIA YA LESENI ZA USAFIRISHAJI

(SURA 317)

KANUNI

# KANUNI ZA (MAGARI YA KUBEBA BIDHAA HATARISHI) ZA SHERIA YA LESENI ZA USAFIRISHAJI ZA MWAKA 2023

## MPANGALIO WA KANUNI

### SEHEMU YA KWANZA
### VIFUNGU VYA AWALI

*Kanuni* *Jina*


1. Jina
2. Matumizi
3. Tafsiri


### SEHEMU YA PILI

### UTOAJI WA LESENI KWA VYOMBO VINAVYOBEBA BIDHAA HATARISHI


4. Vigezo vya utoaji wa Leseni
5. Katazo la kutoa huduma ya kubeba bidhaa hatarishi bila kuwa na Leseni
6. Maombi ya leseni
7. Kukataa kutoa leseni
8. Utoaji wa leseni
9. Kuhuisha leseni
10. Ada ya leseni
11. Utoaji wa kibali cha mpakani


### SEHEMU YA TATU
### WAJIBU WA MWENYE LESENI


12. Wajibu wa kutoa huduma
13. Wasilisho la malalamiko


### SEHEMU YA NNE
### MASHARTI YA LESENI


14. Masharti ya leseni
15. Kuharibika kwa mitambo ya chombo kinachobeba bidhaa hatarishi
16. Kupotea au uharibifu wa leseni
17. Uhalali wa leseni

18. Kusimamishwa au kufutwa
19. Utaratibu wa kufutwa au kusimamishwa
20. Utaratibu wa mapitio

SEHEMU YA SITA
UTUNZAJI NA USAFIRISHAJI WA BIDHAA HATARISHI

21. Utunzaji na usafirishaji wa bidhaa hatarishi
22. Ufungaji wa bidhaa hatari
23. Alama za kuashiria bidhaa hatarishi na maeneo ya kuegesha

SEHEMU YA SABA
VIFUNGU VYA UJUMLA

24. Utozaji kwa kutumia bei elekezi
25. Mamlaka ya kusimamisha na kukagua chombo
26. Kuondolewa kwa chombo kwenye matumizi
27. Kufa au kushindwa kwa mwenye leseni
28. Wajibu wa kutafuta taarifa
29. Wajibu wa kutoa taarifa
30. Ushughulikiaji wa dharura
31. Mafunzo maalum kwa madereva
32. Makosa

JEDWALI

Tangazo la Serikali. ……………….. la tarehe …………………

SHERIA YA LESENI ZA USAFIRISHAJI

(SURA YA 317)

KANUNI

KANUNI ZA (VYOMBO VYA KUBEBA BIDHAA HATARISHI) ZA SHERIA YA LESENI ZA USAFIRISHAJI ZA MWAKA 2023

SEHEMU YA KWANZA
VIFUNGU VYA AWALI

Jina

1. Kanuni hizi zinajulikana kama Sheria ya Leseni za Usafirishaji (Magari ya Kubeba Bidhaa Hatarishi) Kanuni, 2023

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika kwa vyombo vinavyobeba bidhaa hatarishi ndani ya Tanzania Bara na vile vinavyotoa huduma kutoka Tanzania Bara kwenda nchi ya nje

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha unahitaji vinginevyo:

Sura ya 317

"Sheria" ina maanisha Sheria ya Leseni za Usafirishaji;

Sura ya 413

"Mamlaka" ina maanisha Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, iliyoanzishwa chini ya Kifungu cha 4 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini;

"mamlaka husika" maana yake ni mamlaka yenye dhamana ya kushughulikia, kusimamia na kusafirisha bidhaa hatarishi;

"usafirishaji wa kuvuka mipaka" inamaanisha usafirishaji wa mizigo inayovika mipaka;

Sura ya 413

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 15 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini;

" chombo kinachobeba bidhaa hatarishi " maana yake ni chombo cha moto kilichojengwa au kubadilishwa kwa ajili ya kukodishwa, kwa malipo ya moja kwa moja au vinginevyo kwa ajili ya kubeba bidhaa hatarishi au tera lililojengwa kwa ajili ya kubeba bidhaa hatarishi;

"bidhaa hatarishi" maana yake ni dutu yenye uwezo wa kuleta hatari kubwa kwa watu, afya, mali, mazingira na ambayo imeainishwa na mamlaka yenye uwezo na inajumuisha bidhaa za petroli, cyanide, milipuko na kemikali na bidhaa nyingine za aina hiyo;

"bidhaa hatari zinazomwagika" maana yake ni bidhaa hatarishi zinazovuja na kuingia katika ardhi, maji yoyote au sehemu yoyote na kuhatarisha mazingira, maisha au mali;

"Tukio" maana yake ni:

(a) tukio linalohusisha kuvuja kwa bidhaa hatarishi kutoka kwenye chombo cha usafirishaji au kumwagika kwa bidhaa hatarishi zinapokuwa zinasafirishwa;

(b) vifo au majeraha binafsi yanayotokea kutokana na usafirishaji wa bidhaa hatarishi;

(c) tukio la moto linalotokana na usafirishaji wa bidhaa hatarishi; au
(d) tukio lingine lolote kubwa ambalo linaweza kuathiri vibaya mwenendo wa usafirishaji wa bidhaa hatarishi;
"leseni" maana yake ni leseni ya mtoa huduma iliyotolewa chini ya Sheria;
"Mwenye leseni" maana yake ni mtu au kampuni au chama kilichopewa leseni na Mamlaka kutoa huduma ya kusafirishaji wa bidhaa hatarishi zinazobebwa kwa njia ya barabara;
"chombo cha moto" maana yake ni chombo kililokusudiwa au kupitishwa kwa ajili ya kusafirisha bidhaa hatarishi barabarani;
“leseni yenye madhumuni mengi” maana yake ni leseni inayotolewa kwa chombo ambacho kina uwezo wa kubeba bidhaa hatarishi au bidhaa za kawaidi kwa nyakati tofauti, mfano tela la kichanja;
"mtoa huduma" maana yake ni mtu anayemiliki chombo cha moto kinachotumika kubeba bidhaa hatarishi;
"alama za usalama" ina maanisha alama, kifaa, ishara, lebo, bango, barua, neno, idadi ya kifupi, au mchanganyiko wowote wa vitu hivyo, ambayo huonesha aina ya bidhaa hatarishi iliyobebwa kwenye chombo cha moto wakati wote wa safari;
“kifaa cha kufuatilia chombo cha moto" maana yake ni kifaa kilichofungwa kwenye chombo cha moto kinachosafirisha bidhaa hatarishi chenye uwezo wa kupokea na kusambaza wa kusambaza taarifa kwa wakati halisi kwa Mfumo wa Ufuatiliaji wa Magari au kifupi chake "VTS"

## SEHEMU YA PILI
## UTOAJI WA LESENI KWA VYOMBO VINAVYOBEBA BIDHAA HATARISHI

Vigezo vya utoaji wa Leseni

4. (1) Mamlaka inaweza kutoa leseni kwa mtu au kampuni kuendesha chombo ambacho kinabeba bidhaa hatarishi.
(2) Mamlaka itatoa Leseni endapo mwombaji ni-
(a) raia wa Tanzania au kampuni iliyosajiliwa chini ya sheria za Tanzania; na
(b) imekidhi viwango, vigezo na masharti ya utoaji wa huduma za ubebaji na usafirishaji wa bidhaa hatarishi kwa namna itakavyoainishwa;

Katazo la Kutoa huduma ya kubeba bidhaa hatarishi bila kuwa na leseni

5. Mtu yeyote hataruhusiwa kufanya shughuli za usafirishaji wa bidhaa hatarishi bila leseni halali iliyotolewa na Mamlaka kwa mujibu wa Kanuni hizi.

Maombi ya leseni

6. (1) Mtu yoyote anayekusudia kutoa huduma za usafirishaji wa bidhaa hatarishi anatakiwa kuomba leseni kwa Mamlaka kupitia fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili na atalipa ada zilizoainishwa katika Jedwali la tatu la Kanuni hizi.
(2) Maombi chini ya kanuni ndogo ya (1), yataambatana na-
(a) nakala ya kadi ya usajili wa chombo cha moto;
(b) Taarifa ya ukaguzi wa chombo cha moto; na
(c) Taarifa ya matakwa ya kiufundi.
(3) Endapo muombaji ni kampuni, atatakiwa kuwasilisha nyaraka za ziada zifuatazo-
(a) nakala ya cheti cha kusajiliwa;
(b) Mpango wa Usimamizi wa Usalama;
(c) Mpango wa kukabiliana na dharura; na
(d) Nyaraka nyingine yoyote ambazo Mamlaka inaweza kuhitaji wakati wowote.

Kukataa kutoa leseni

7. (1) Mamlaka ina uwezo wa kukataa kutoa leseni endapo hajatimiza matakwa yaliyoainishwa chini ya Kanuni hizi;

(2) Endapo Mamlaka itakataa kutoa leseni, itamtaarifu kwa maandishi mwombaji sababu za kukataliwa ndani ya siku kumi na nne tangu kupokea maombi hayo.

Utoaji wa Leseni

8. (1) Endapo Mamlaka itajiridhisha kuwa maombi ya leseni yamekidhi matakwa ya Kanuni hizi, itatoa leseni.

(2) Leseni itakayotolewa chini ya kanuni hii itakuwa na yafuatayo-

(a) jina na anwani ya mwenye leseni;

(b) namba za usajili wa chombo cha moto kinachobeba bidhaa hatarishi;

(c) aina ya bidhaa hatarishi inayotakiwa kubebwa;

(d) muda wa leseni;

(e) kiwango cha juu cha mzigo kilichoidhinishwa kubebwa; na

(f) Masharti ya leseni.

(3) Mamlaka inaweza kutoa leseni yenye madhumini mengi kwa mtu au kampuni inayodhamiria kufanya shughuli za usafirishaji wa bidhaa hatarishi au bidhaa za kawaida iwapo shughuli hizi hazitafanyika kwa pamoja.

Kuhuisha leseni

9. (1) Mwenye leseni anayehuisha leseni anatakiwa kufanya hivyo ndani ya siku thelathini kabla ya leseni yake kuisha;

(2) Maombi ya kuhuisha leseni yataambatana na-

(a) uthibitisho wa malipo ya tozo ya Mamlaka kwa mwaka uliotangulia; na

(c) cheti halali cha ubora wa chombo.

(3) Mamlaka inaweza kutoza asilimia hamsini ya ada ya leseni kwa maombi yaliyowasilishwa siku kumi na nne baada ya tarehe ya kumalizika muda wa leseni na asilimia tano kwa kila mwezi unaofuata kwa salio lililolimbikizwa kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili.

(4) Mamlaka haitashughulikia maombi ya kuhuisha leseni endapo leseni iliyoisha ina madeni hadi yatakapolipwa.

Ada ya leseni

10. Mwombaji wa leseni atalipa ada ya Mamlaka kama ilivyoainishwa katika Jedwali ya Tatu la Kanuni hizi.

Utoaji wa kibali cha mpakani

11. (1) Mamlaka itatoa kibali kwa mwenye leseni ya chombo cha moto anayekusudia kubeba bidhaa hatarishi kuvuka mpaka wa nchi.

(2) Maombi ya kibali cha kuvuka mipaka yataambatana na-

(a) Leseni halali iliyotolewa chini ya Kanuni hizi; na

(b) maelezo ya ruti inayotumika mpaka mwisho wa safari.

(3) Muda wa kibali kinachotolewa chini ya kanuni hii hautazidi muda wa uhai wa leseni.

## SEHEMU YA TATU
## WAJIBU WA MWENYE LESENI

Wajibu wa kutoa huduma

Sura ya 413.

12. Mwenye Leseni ya usafirishaji wa bidhaa hatarishi anapaswa-

(i) kuingia katika mkataba wa huduma na mteja;

(ii) kutoa huduma kulingana na vigezo na masharti vilivyoainishwa katika mkataba;

(iii) kutoa au kusababisha kutoa risiti itakayoonesha yafuatayo-

(a) jina kamili la mteja

(b) anuani na namba ya simu ya mwenye leseni

(c) aina ya bidhaa hatarishi

(d) kiasi cha fedha cha kusafirisha bidhaa hatarishi

(e) tarehe inayotarajiwa kufikisha kwa bidhaa hatarishi

(f) tarehe ya kutolewa stakabadhi
(g) jina na sahihi ya Afisa aliyetoa stakabadhi

Kuwasilisha malalamiko

13. Mtu ambaye hataridhika na huduma inayotolewa na mwenye leseni anaweza kuwasilisha malalamiko kwa Mamlaka kama ilivyoainishwa katika kanuni -----

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA LESENI

Masharti ya leseni

14. Mwenye leseni atahakikisha kuwa-

(a) chombo chenye leseni kinatunzwa na kuwekwa kwenye hali nzuri;
(b) dereva wa chombo amethibitishwa na Mamlaka;
(c) chombo kinachobeba bidhaa hatarishi kinazingatia ubora uliowekwa na mamlaka inayohusika na masuala ya viwango nchini;
(d) chombo kinafuata sheria za barabarani na sheria nyingine zozote zinazohusika na usafirishaji wa bidhaa hatarishi;
(e) abiria hawasafirishwi katika chombo kinachobeba bidhaa hatarishi;
(f) chombo chenye uwezo wa kubeba tani tatu na zaidi kiwe kimefungwa kifaa cha mfumo wa kufuatilia mwenendo wa chombo;
(g) chombo kinachobeba bidhaa hatarishi kiwe kimewekewa alama stahiki za tahadhari kwa mujibu wa utaratibu wa tasnia husika; na
(h) chombo kinachobeba bidhaa hatarishi hakitelekezwi.

Kuharibika kwa chombo kinachobeba bidhaa hatari

15. Endapo chombo chenye leseni kikashindwa kuendelea na safari kutokana na sababu za kiufundi, mwenye leseni atalazimika kutoa usafiri mbadala wa kusafirisha bidhaa hatarishi ndani ya masaa kumi na mbili.

16. (1) Pale leseni itakapo-
(a) haribika mwenye leseni atapeleka mara moja taarifa ya maandishi kwa Mamlaka pamoja na maombi ya kubadilishiwa; au
(b) potea, mwenye leseni ataitaarifu Mamlaka kwa maandishi na kuambatisha taarifa ya Polisi ya upotevu wa leseni hiyo na kuomba leseni durufu.

(2) Mamlaka itakapojiridhisha kuwa leseni imepotea, kuharibiwa au vinginevyo, itatoa nakala durufu ya leseni, baada ya mwenye leseni kufanya malipo ya ada inayostahiki,

Isipokuwa kwa leseni zilizoharibika, mwenye leseni atatakiwa kuwasilisha nakala iliyoharibika kwa ajili ya uhakiki kabla ya kupewa leseni durufu.

(3) Endapo leseni iliyopotea ikapatikana wakati Mamlaka imeshatoa Leseni durufu, mtoa huduma atapaswa kurudisha leseni durufu kwa Mamlaka.

Uhalali wa leseni

17. (1) Leseni iliyotolewa chini ya Kanuni hizi itakuwa halali kwa kipindi cha mwaka mmoja na inaweza kuhuishwa kila mwaka.

(2) mwenye leseni atakayeshindwa kutoa huduma kwa muda unaozidi siku thelathini ataitaarifu Mamlaka kwa maandishi.

Kusimamishwa au kufuta leseni

18. (1) Endapo mwenye leseni atakiuka vigezo na masharti ya leseni, Mamlaka ita-

(a) sitisha au kufuta leseni au kibali; na
(b) mjulisha mwenye leseni au kibali kuwa leseni yake au kibali chake kimesimamishwa au kufutwa na sababu za kusimamishwa au kufutwa kwa

shughuli hiyo zitaelezwa kwa maandishi.

(2) Mamlaka itarudisha leseni kwa mwenye leseni baada ya kumalizika kwa muda wa kusimamishwa na kutimiza masharti mengine kama yalivyoainishwa na Mamlaka.

Utaratibu wa kufuta au kusimamishwa

19. (1) Mamlaka inatakiwa kabla ya kusimamisha au kufuta leseni au kibali, kutuma taarifa ya kumtaka ajieleze kwa nini asifungiwe au kusimamishiwa leseni au kibali chake.

(2) Mwenye leseni, baada ya kupokea taarifa katika kanuni ndogo ya (1), atatoa maelezo kwa maandishi kwa Mamlaka ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya kupokea taarifa inayoonesha sababu kwa nini leseni isifutwe au kusimamishwa.

(3) Mamlaka inaweza kufuta au kusimamisha leseni au kibali na kutoa sababu pale ambapo-

(a) Mamlaka haijaridhika na maelezo yaliyotolewa chini ya Kanuni ndogo ya (2); au

(b) Mwenye leseni hajatoa maelezo yoyote.

(4) Endapo leseni itasitishwa au kufutwa chini ya Kanuni hizi, mwenye leseni ataacha mara moja kutoa huduma za usafiri na atasalimisha leseni kwa Mamlaka ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya kupokea taarifa ya kusimamishwa au kufutwa.

(5) endapo leseni itabaki kuwa hai baada ya kumaliza kipindi cha kusimamishwa na kukidhi matakwa mengine aliyopewa wakati wa kusimamishwa, Mamlaka itarudisha leseni hiyo kwa mtoa huduma.

## SEHEMU YA TANO
## UTUNZAJI NA USAFIRISHAJI WA BIDHAA HATARISHI

Utunzaji na usafirishaji wa bidhaa hatarishi

20. (1) Mtu yoyote hataruhusiwa kutoa au kupokea bidhaa hatarishi kwa ajili ya kuisafirisha kwa njia ya barabara endapo bidhaa hizo hazijaainisha au kuwekewa alama za usalama na kudhibitishwa kwenye nyaraka za usafirishaji.

(2) Mtu yoyote hatoruhusiwa kusafirisha bidhaa yoyote hatarishi zitakazoonekana kuwa na makosa katika uwekaji alama au nyaraka.

Ufungaji wa bidhaa hatarishi

21. (1) Maelezo ya ufungaji yanayotumika kwenye bidhaa hatarishi za daraja la 1 hadi 9 yaliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi yatakuwa kama yalivyoainishwa katika sheria za Kimataifa za Bidhaa Hatarishi za Majini (1965).

(2) Mtu yeyote anayedhamiria kusafirisha bidhaa hatarishi ambazo hazijaidhinishwa hasa katika maelekezo ya ufungaji wa bidhaa hatarishi ataomba kibali kutoka kwa mamlaka husika.

Alama za kuashiria bidhaa hatarishi na maeneo ya maegesho

22. (1) Msafirishaji wa bidhaa hatarishi atahakikisha kuwa-

(a) bidhaa hatarishi zilizobebwa zinawekwa alama inayoonekana kirahisi na watumiaji wengine wa barabara juu ya uhatari uliyopo katika bidhaa kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.

(b) alama zinazowekwa kwenye bidhaa hatarishi zina uwezo wa kuhimili hali ya hewa yoyote bila kuathiri rangi, aina na muundo wa alama husika.

(c) maeneo ya maegesho atakayoyatumia kwa muda wakati akiwa safarini yana usalama na hayawezi kuingiliwa kirahisi na watumiaji wengine wa barabara.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI YA UJUMLA

Utozaji wa tozo elekezi

23. Kulingana na masharti yaliyowekwa na Kanuni hizi, mwenye leseni atatoza wateja wake kiasi kisichozidi kile ambacho kimeidhinishwa na Mamlaka.

mamlaka ya kusimamisha na kukagua chombo

24. Afisa aliyeidhinishwa anaweza kusimamisha na kukagua chombo ili kubaini iwapo Kanuni hizi zinazingatiwa na anaweza kutaka kuoneshwa leseni au nyaraka nyingine zozote ambazo zinapawa kuwa kwenye chombo wakati wote wa safari.

kuondoa chombo kwenye matumizi

25. Endapo mwenye leseni ataondoa chombo kinachohusika na leseni kwenye matumizi au kukoma kuwa mmiliki wa chombo atapaswa kuitaarifu Mamlaka na kurejesha leseni ndani ya siku saba.

kifo au kukosa uwezo kwa mwenye leseni

26. Mtu atakayekusudia kufanya biashara kwa niaba ya mwenye leseni aliyefariki au kukosa uwezo, kufilisika au kukoma kutumia leseni, atatakiwa-

(a) Kuitaarifu Mamlaka kuwa mwenye leseni amekoma kuwa mmiliki wa chombo ndani ya siku thelathini baada ya kifo au kukosa uwezo na kutoa taaria ya jina la mtu ambaye anaendesha biashara; na

(b) kuomba leseni mpya ndani ya mwezi mmoja baada ya kutoa taarifa kwa Mamlaka.

Isipokuwa kwamba katika kipindi ambacho Mtu huyo atachukuliwa kama mwenye leseni hatapaswa kuendelea kuitumia leseni hiyo baada ya muda wake kuisha.

Wajibu wa kutafuta taarifa

27. Mtu ambaye anadhamilia kumiliki chombo au kuajiri dereva anapaswa kuomba taarifa kwa Mamlaka ili kuweza kupata taarifa halisi za chombo hicho au dereva huyo.

Wajibu wa kutoa taarifa

28. (1) Mwenye leseni anatakiwa kutoa taarifa kwa Mamlaka ndani ya siku thelathini kuhusu mabadiliko ya anuani ya ofisi na taarifa nyingine zozote au mabadiliko ya masuala yoyote ambayo yalikuwa katika uombaji wa leseni.

(2) Mwenye leseni anapaswa kuitaarifu Mamlaka kuhusu tukio lolote litakalotokea wakati wa kusafirisha bidhaa hatarishi kabla ya saa ishirini na nne baada ya tukio kutokea.

Huduma ya dharura

29. Msafirishaji wa bidhaa hatarishi anapaswa kuwa na mpango wa huduma ya dharura kwa ajili ya ajali na matukio.

Mafunzo maalum kwa madereva

30. Dereva hataruhusiwa kuendesha au kuhudumia chombo kilichobeba bidhaa hatarishi isipokuwa amepatiwa mafunzo maalum au yupo chini ya uangalizi wa dereva ambaye amepata mafunzo ya kuhudumia au kuendesha kutoka katika chuo kinachotambulika.

Makosa

31. Mtu atakayekiuka masharti ya kanuni hizi atakuwa ametenda kosa na pale atakapopatikana na hatia atatakiwa kulipa faini isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi shilingi milioni tatu au kifungo cha kipindi kisichopungua miezi mitatu na kusichozidi mwaka mmoja au vyote.

Mapitio
TS. Na. 73 ya mwaka 2020

32. Mtu ambaye hataridhika na uamuzi wa Mamlaka atatuma maombi ya mapitio kulingana na Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Utaratibu wa mapitio) za mwaka 2020.

JEDWALI LA KWANZA

*(Imetungwa chini ya Kanuni 21(1))*

**AINA ZA BIDHAA NA VITU HATARISHI**

**(a) Darasa la 1: Vilipuzi**

Mgawanyiko 1.1: Vitu na makala ambazo zina hatari ya mlipuko mkubwa
Mgawanyiko 1.2: Vitu na makala ambazo zina hatari ya makadirio lakini sio mlipuko mkubwa
Hatari
Mgawanyiko 1.3: Vitu na makala ambazo zina hatari ya moto na ama hatari ndogo ya mlipuko au hatari ndogo ya makadirio au zote mbili, lakini sio hatari ya mlipuko mkubwa
Mgawanyiko 1.4: Vitu na makala ambazo hazina hatari kubwa
Mgawanyiko 1.5: Vitu visivyojali sana ambavyo vina hatari kubwa ya mlipuko
Mgawanyiko 1.6: Makala zisizo na maana sana ambazo hazina hatari ya mlipuko mkubwa

**(b) Daraja la 2: Gesi**

Mgawanyiko 2.1: Gesi zinazoweza kuwaka
Mgawanyiko 2.2: Gesi zisizo na sumu, zisizo na sumu
Mgawanyiko 2.3: Gesi zenye sumu

**(c) Darasa la 3: Vimiminika vinavyoweza kuwaka**

**(d) Darasa la 4: Imara zinazoweza kuwaka; vitu vinavyohusika na mwako wa hiari; vitu ambavyo, kwa kuwasiliana na maji, hutoa gesi zinazoweza kuwaka**

Mgawanyiko 4.1: Vitu vinavyoweza kuharibika, vitu vinavyojitegemea na milipuko imara iliyoharibika
Mgawanyiko 4.2: Vitu vinavyohusika na mwako wa hiari
Mgawanyiko 4.3: Vitu vinavyogusana na maji hutoa gesi za moto

**(e) Darasa la 5: Oxidizing dutu na peroxides ya kikaboni**

Mgawanyiko 5.1: Oxidizing vitu
Mgawanyiko 5.2: Peroksidi za kikabon

**Darasa la 6: Vitu vyenye sumu na kuambukiza**

Mgawanyiko 6.1: Vitu vyenye sumu
Mgawanyiko 6.2: Vitu vya kuambukiza

**(f) Darasa la 7: Nyenzo za mionzi**

**(g) Darasa la 8: Vitu vyenye kutu**

**(h) Darasa la 9: Vitu na makala hatarishi**

*****Kwa bidhaa na vitu hatarishi, si vinginevyo vilivyoainishwa, consignor atashauriana na mamlaka yenye uwezo.

JEDWALI LA PILI

(Zimetengenezwa chini ya Kanuni 6(1)

MAOMBI YA LESENI YA USAFIRISHAJI
WA BIDHAA HATARISHI

Asili ya Maombi: ☐ Mpya ☐ Kuhuisha ☐ Kubadilisha ☐

Kipindi kinachoombwa kwa: ☐

A. MAELEZO YA MUOMBAJI

1. Jina la biashara kamili ………………………………………
   (Kampuni/Ubia/ Biashara mtu mmoja Sole Trader- KWA HERUFI KUBWA)
2. Anwani …… Simu ……
   Nukushi: ……… Tovuti: ……………
3. Unamiliki au ushawahi kuwa na leseni ya usafirishaji? …Ndiyo/Hapana
   Ikiwa Ndiyo, Taja namba ya leseni ……… na tarehe ya kuisha …………………………na ilipotolewa .
4. Ushawahi kuwa na maombi yaliyokataliwa /kusimamishwa au kufutwa ?……Ndiyo/Hapana
   Ikiwa Ndiyo, eleza linin a wapi maombi yalikataliwa, simamishwa, au kufutwa yalifanyika ………, Eleza sababu ya maombi kukataliwa, leseni kusimamishwa au kukataliwa : ………….. na tarehe ………………………

B. MAELEZO YA GARI AMBALO LESENI INAOMBWA

(i. Usajili. Na: ☐ ii. Toleo: ☐

iii. Aina : ☐ iv. Mji ☐

(v) Gari ☐ ☐

(b) Idadi ya ekseli zinazobeba na chombo

☐ Kongosho Tembo ☐ Gari Eksel 3+ ☐ Tera kubwa Tera dogo

☐ Gari ya ekse ☐ Gari ya ekseli ☐

c) Daraja na aina za bidhaa hatarishi
…………………………………………………………………………

vi. Uwezo wa kubeba
……………………………………………………

C. NYARAKA ZA KUWEKA

Maombi hii lazima iambatane na vitu vilivyoorodheshwa hapa chini. Leseni inaweza kuhitaji maelezo zaidi.

(1) MOMBI MAPYA

(a) nakala ya kadi ya usajili wa magari
(b) bima ya bima, angalau kufunika mtu wa tatu.
(c) Ripoti ya ukaguzi wa lazima wa gari.
(d) Ripoti ya maelezo ya kiufundi.
(e) Mpango wa Usimamizi wa Usalama;
(f) Cheti cha ustahili wa barabara za magari; Na
(g) Hati nyingine yoyote ambayo inaweza kuombwa na Mamlaka.

Nyaraka za ziada katika kesi ya kampuni
(a) nakala ya cheti cha kuingizwa;
(b) Mpango wa Usimamizi wa Usalama;
(c) Mpango wa kukabiliana na dharura; Na
(d) Nyaraka nyingine yoyote kama Mamlaka inaweza kuhitaji.

(2) KUHUISHA

(a) nakala ya kadi ya usajili wa magari;

(b) Taarifa ya ukaguzi wa lazima wa magari;

(c) bima inashughulikia angalau kufunika mtu wa tatu;

(d) Taarifa ya vipimo vya kiufundi; Na

(e) Hati nyingine yoyote kama Mamlaka inaweza kuhitaji.

D. TAMKO

Mimi/.................................... hapa tangaza kwamba kwa ufahamu wangu wote / ufahamu wetu habari zote zinazotolewa katika programu hii ni kweli.

Sahihi: ……………………………… Tarehe: ………………………

KWA MATUMIZI YA OFISI TU

| | | |
|---|---|---|
| Kiasi kilicholipwa:<br>………………………… | Risiti Na.<br>…………………. | Tarehe:<br>……………….……<br>Sahihi:<br>………………… |

| | |
|---|---|
| Uhakiki na Mapendekezo<br>omments:<br>Tarehe ya kuanza: … Tarehe ya kuisha:<br><br>Jina kamili rasmi: ……………………<br>Wasifu: …………………………<br>Sahihi: …………… Tarehe : ………… | kuidhinishwa<br>maoni<br>Tarehe ya kuanza: … Tarehe ya kuisha:<br>……………<br>Jina rasmi kamili:<br>…………………..<br>… Wsifu:<br>…………………………………<br>Sahihi: ………………….….. |

| | | |
|---|---|---|
| JINA LA MWENDESHAJI<br>NAMBA<br><br>………………………. | NAMBA YA LESENI<br><br>…………………… | KITAMBU<br>LISHO |

---

JEDWALI LA TATU

---

(Zimetengenezwa chini ya Kanuni 10)

JEDWALI LA ADA YA LESENI KWA MAGARI YA
WASAFIRISHAJI WA BIDHAA HATARISHI NDANI NA NJE YA NCHI
.

| S/n | Maelezo | Ada mwaka Tshs | Ada mwaka US $ |
|---|---|---|---|
| 1 | Isiyozidi tani moja | 10,000/= | 20 |
| 2 | Kuanzia tani 1 hadi tani 5 | 20,000/= | 50 |
| 3 | Kuanzia tani 5 hadi tani 9.9 | 45,000/= | 95 |
| 4 | Kuanzia tani 10 hadi 14.9 | 50,000/= | 115 |
| 5 | Kuanzia tani 15 hadi tani 19.9 | 75,000/= | 160 |
| 6 | Kuanzia tani 20 hadi tani 24.9 | 90,000/= | 195 |
| 7 | Kuanzia tani 25 hadi tani 29.9 | 110,000/= | 230 |
| 8 | Kuanzia tani 30 na zaidi | 120,000/= | 250 |

Angalizo:
Ada inategemea uwezo wa chombo cha moto kubeba mzigo na na sio uzito wa chombo. Magari yote yamewekwa pamoja bila kujali hadhi yao ikiwa peke yake au na tera.

Ada/gharama

1. Fomu ya maombi .................................................................... 10,000/= (10 USD)
2. Nakala ya leseni iliyopotea, iliyoharibiwa
   au Kuchafuliwa …………………….............……….........20,000/= (15USD)
3. Ada ya maombi ya vibali vya mipakani ................................ 50,000/= (50 USD)
4. Cheti cha utambuzi wa kampuni ya
   usafirishaji . ..........................................................................100, 000/= (100 USD)

---

Dodoma,
………...., 2023

Makame Mbarawa,
*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi*